Husein رضي الله عنه
Na Biashara Ya Damu Yake

Mtunzi
Ibrahim Al Ajlani

www.dd-sunnah.net

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Damu inamwagika, Kelele na Vilio.....! Nguo zinachanwa, Nyuso zinapigwa.....! (na kuimbwa) mashairi ya maombolezo, pamoja na kudhihirisha huzuni.

Kujipiga kichwani na huku zikisikika sauti za masikitiko: Ewe Husein Ewe Husein! Kwa ajili ya kuwatisha na kuwakemea waliomuua shahidi (Husein (Allah amridhie).....

Hakika hizi ni kumbukumbu zenye kujikariri (kila mwaka) zinazofanywa na kundi la Shia (Raafidhwah), mpaka limekuwa tukio hilo ni miongoni mwa misingi ya Madhehebu ya Shia (Raafidhwah) katika kila sehemu: kujiliza kwa madai ya kutetea damu ya Husein ibn Aliﷺ.

Na katika historia ya binadamu halijawahi kupatikana tukio lolote la ki-biashara na kujikusanyia pesa kwa kujiliza (kilio cha uwongo) kama ilivyo katika tukio la kuuawa Huseinﷺ.

Hakika Mashia wameikuza sura ya msiba huu Zaidi katika maisha yao, kuliko zinavyoeleza dalili za kisheria ambazo tunazijua kuhusu kuuliwa kwake (Huseinﷺ) hali ya kuwa shahidi.

Tukio hilo ni sehemu ya **kujikusanyia watu**, **na ni Sindano (yenye kuathiri) kwenye nafsi za wafuasi wao, na kuinunua mioyo** kwa kutumia jina la kudhulumiwa.

Siku za nyuma tukio hili lilikuwa na taswira ya ki-madhehebu, lakini kwa sasa hivi limeshika nafasi ya ki-siasa; mpaka limefanywa kuwa ni (tukio) kubwa kuliko mauaji (yaliyofanywa na) Wagiriki na Warumi (dhidi ya waislamu), na pia linafanana na simulizi za Ki-giriki kwa kukusanya riwaya za uwongo na ngano za kale.

Kwa ajili hiyo risala hii imeandikwa ili umjue Huseinﷺ, na kujua maisha, habari zake, pamoja na kuuliwa kwake hali ya kuwa ni shahidi; na ili tufahamu nani ana haki zaidi kwa Huseinﷺ?, nani aliyemhadaa Huseinﷺ?, kisha (tujue) ni upi msimamo wa Ahlus Sunnah kuhusu tukio hili na yale yanayo fungamana nayo. Nani ambae analifanya (tukio hili) kuwa ni biashara, ni wapi?, Na kwa namna gani?.

MWANZO WA KISA:

Wakati Mtume ﷺ alipopata habari ya kwamba binti yake Fatma (Allah amridhie) amezaa mtoto alipatwa na mshangao, kisha akatoka kwa haraka na huku kikoi chake kinaburuta chini.

Akaingia nyumbani kwa Fatma (Allah amridhie) na kumpongeza, kisha akambeba mtoto huyo kwa mikono yake, baada ya hapo ikaletwa tende na Mtume ﷺ akaitia mdomoni na kuitafuna kisha akamrambisha kwa mate yake, kisha akamuuliza Aliﷺ: **umempa jina gani?** Aliﷺ akajibu: **(nimemwita) Ja'far**, Mtume ﷺ akamchagulia jina ambalo hawakuwa watu wakiitana kabla ya hapo, akasema: **(mwite Husein)**,

na alipofika siku ya saba tangu kuzaliwa kwake alifanyiwa A'qiqa na babu yake ambaye ni Mtume ﷺ kwa kuchinjiwa mbuzi wawili.

Aliishi mtoto huyu na kukulia katika nyumba ya Mtume ﷺ ambayo Allah amewasifu watu wake) kwa kusema:

﴿إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجْسَ أَهْلَ ٱلْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا﴾

(Hakika Allah anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume na kukusafisheni vizuri)[1].

Kwa hakika moyo wa Mtume ﷺ ulijaa mapenzi na huruma kubwa kwa mtoto huyu mpaka akamuita: RAYHANA (mmea ulio na harufu nzuri), bali mapenzi yalikuwa makubwa kiasi cha kushindwa kuvumilia wakati anaposikia Husein رضي الله عنه analia.

Siku moja Mtume ﷺ alipita nyumbani kwa Ali رضي الله عنه akamsikia Husein رضي الله عنه analia akasema kumwambia Fatma (Allah amridhie).

«أَلَمْ تَعْلَمِي أَنَّ بُكَاءَهُ يُؤْذِينِي؟»

[hivi hukujua kwamba kilio chake kinaniudhi]?[2].

Husein رضي الله عنه alipokuwa mkubwa (kidogo) alikuwa mara kwa mara anaenda msikitini kwa hamu ya kumwona babu yake (Mtume ﷺ), akawa kijana huyu mdogo ana mafungamano makubwa na babu yake, alikuwa anaposikia tu sauti

yake basi moyo wake unamhurumia (kijana huyo) kisha anamfuata na kucheza nae, na anapata kutoka kwake huruma ya mzazi.

Vimetusimulia vitabu vya hadithi ya kwamba siku moja Mtume ﷺ akiwa anahutubia Maswahaba zake, akaingia Hasan na Husein (Allah awaridhie) wakiwa wamevaa nguo nyekundu, wanatembea huku wakianguka, Mtume ﷺ alipoona hali hiyo alishindwa kusubiri, alikatisha hotuba na kuteremka katika mimbari yake na akawaelekea, akawakumbatia kisha akapanda nao katika mimbari, akasema: amesema kweli Allah:

﴿إِنَّمَآ أَمْوَٰلُكُمْ وَأَوْلَٰدُكُمْ فِتْنَةٌ﴾

(Hakika mali yenu na watoto wenu ni mtihani)[3].

Kisha akasema: **[Nimewatazama na sikuweza kuvumilia]**, kisha akaendelea na hotuba yake[4].

Bali mara nyingine Husein رضي الله عنه akiingia katika msikiti wa Mtume ﷺ na kumpandia juu ya mgongo wake na hali ya kuwa Mtume ﷺ amesujudu, na alikuwa anarefusha sijda hiyo ili asije kumharakisha[5] (akakata starehe yake).

Siku moja Mtume ﷺ (alitoka kwenda (sehemu fulani) kwa ajili ya

---

1 - Surat Al-Ahzaab/33.

2 - Hadithi ameipokea Imam Twabrany katika Mu'jamul kabiir: (J: 3, Uk: 116) hadithi namba (2847), amesema sheikh Abdur Rahman As Suhaymiy: (hadithi hii ni dhaifu).

3 - Surat At Taghaabun/15.

4 - Ameipokea imamu Ahmad (J: 38, Uk: 100), namba (22995), na ameisahihisha Ibn Khuzaymah (J: 2, Uk: 355), na Ibn Hibbaan (J: 13, Uk: 402), na Al Haakim (J: 1, Uk: 286).

5 - Ameipokea imamu Ahmad (J: 45, Uk: 613), namba (27648) kwa sanadi sahihi.

chakula, mara njiani akamwona Husein ﷺ anacheza, Mtume ﷺ (alimfuata na akanyoosha mikono yake, Husein ﷺ akawa anakimbia huku na huku (anacheza) na huku Mtume ﷺ akimchekesha, kisha akambeba na akasema:

[Husein anatokana na mimi na mimi natokana na Husein, Allah ampende yule atakaempenda Husein, Husein ni mjukuu wangu[12].

Na inamtosha Husein ibn Ali (Allah awaridhie) kwa utukufu na ubora kauli ya Mtume ﷺ :

(الحَسَنُ وَالحُسَيْنُ سَيِّدَا شَبَابِ أَهْلِ الجَنَّةِ)

(Hasan na Husein ni **mabwana wa vijana wa peponi)**[3].

Enyi watu wa nyumba ya **Mtume kupendwa nyinyi**
Ni faradhi **kutoka kwa Allah aliyoiteremsha kwenye Qur'an**
Inakutosheni nyinyi kuwa **ni wabora kwa sababu**
Yule asiyewaswalia hatorehemewa

Na kabla ya kufariki Mtume ﷺ kwa muda mfupi hakusahau kumuaga Husein na kaka yake Hasan ﷺ kwa kuwakumbatia, kisha akausia kwao kheri[4].

Wakati alipofika umri wa miaka sita Husein ﷺ alipata maumivu kwa kufiwa na babu yake, alihuzunika sana; kwani alikuwa ni mlezi na ni baba mwenye huruma kubwa kwake, baada ya kupita miezi sita huzuni ikarudi tena kwenye moyo wake, kwani alipatwa na tukio kubwa la kushtukiza kwa kufiwa na mama yake Fatma (Allah amridhie).

Baada ya hapo Husein ﷺ aliishi maisha mazuri, kwani maswahaba walikuwa wanamfanyia ukarimu na wanampenda mapenzi makubwa kwa (wasia wa) Mtume ﷺ, na walikuwa wakimwona wanamkumbuka Mtume ﷺ kwa sababu alikuwa amefanana mno kwa sura na babu yake.

Hakika Abubakri Swiddiiq ﷺ alitekeleza ahadi ya swahiba wake (Mtume ﷺ, pamoja kuwa ni (mtu mzima) mwenye miaka sitini alikuwa anamhurumia na kumnyenyekea mno Husein ﷺ); alikuwa anapomwona humfuata na kumfurahia na huku anawaambia watu: **(mchungeni Muhammad kwa 'kuwapenda' jamaa zake)**[5].

Siku moja Abubakri ﷺ alilia huku anamwambia Ali: **(kuwaunga ndugu wa Mtume ﷺ inapendeza zaidi kwangu mimi kuliko ndugu zangu)**[6].

Ama Umar Al Farouq ﷺ alikuwa anamtukuza sana Husein ﷺ anamheshimu, na anampenda, hasa ukizingatia kuwa ni Shemeji yake,

---

1 - Ameipokea Tirmidhiy (J: 5, Uk 658), namba (3775), na ameisahihisha ibn Hibbaan (J: 15, Uk: 427), na sheikh Albany katika (Sahihi Sunani Tirmidhiy), namba (2970).

2 - Hadithi inahimiza juu ya kumpenda Husein (Allah amridhie), na si kwamba Husein ni sawa na Mtume ﷺ.

3 - Ameipokea Ahmad (J: 17, Uk 31), namba (10999), nayo ni hadithi sahihi.

4 - Angalia [Ar Rahiiqul Makhtuum (Uk: 465).

5 - Ameipokea Bukhari (j 5, uk 26), namba (3751).

6 - Bukhari (J: 5, Uk: 20), namba (3711), na Muslim (J: 3, Uk 1380), namba (1759).

kwa sababu Umarﷺ alimuoa ndugu yake Huseinﷺ ambaye ni Ummu Kulthum bint Ali (Allah awaridhie)[1].

Na wakati Umarﷺ alipoanzisha Diwani[2] alikuwa anampa Hasan na Husein (Allah awaridhie) kiasi sawa na anachowapa watu (waliopigana) vita vya Badri; kwa ajili ya kuwapenda na kuwakirimu wajukuu wa (Mtume ﷺ)[3].

Bali siku moja Umarﷺ aliwagawia nguo watoto wa Maswahaba zikamalizika kabla ya kupata Hasan na Husein (Allah awaridhie), Umarﷺ akamtuma mtu kwenda Yemen wakaletewa nguo zao maalumu, kisha akasema: **(Hivi sasa nafsi yangu imefurahi)**[4].

Waislamu waliifungua Miji ya Fursi wakaja na bint wa Mfalme wa (Fursi) Yazdajirdi kwa Umar (Allah amridhie) na alikuwa ni (mwanamke mzuri), Umar (Allah amridhie) hakuipendelea nafsi yake wala yeyote miongoni mwa jamaa zake, lakini alimtoa zawadi kwa mtu anaempenda zaidi, (ambaye ni) Husein ibn Ali (Allah awaridhie), akamuoa na akazaa nae mtoto anayeitwa Ali ibn Husein (Zainul Aa'bidiin), nae ni mtoto pekee wa Husein (Allah amridhie) aliyebaki hai[5].

Kisha akaja Uthmanﷺ akaendeleza kwa Huseinﷺ heshima na kumtukuza, na alikuwa nae karibu zaidi kwa kuwa ni ndugu; kwa sababu Uthamanﷺ aliwaoa Khalat (mama zake wadogo) Huseinﷺ ambao ni Ruqayyah na Ummu Kulthum (Allah awaridhie), watoto wa Mtume ﷺ.

Na vilevile Huseinﷺ aliishi maisha ya na kukirimiwa katika zama za Muawiyahﷺ, alikuwa akiwapa Hasan na Husein (Allah awaridhie) kiasi kikubwa cha pesa[6].

Na Huseinﷺ alikuwa na utukufu kwa kuwa miongoni mwa jeshi ambalo Muawiyah (Allah amridhie) alilituma kwenda kufungua Mji wa Costantinople (Istanbul), jeshi ambalo Mtume ﷺ alisema: **[Jeshi la kwanza katika umma wangu ambalo litapigana katika Mji wa Keiser (Qayswar) limesamehewa]**[7].

Hivi ndivyo yalivyokuwa mapenzi ya baki ya Maswahaba kwa Huseinﷺ, alikuwa Ibn A'bbasﷺ anamshika mnyama wa Huseinﷺ) pindi anapotaka kupanda na anamuona (Husein) kuwa ni miongoni mwa neema kwake[8].

Na swahaba A'mru ibnul 'Aaswiﷺ siku moja alimwona Husein ibn

---

1 - Taareikhu Rrusul wal Muluuk (J: 2, Uk: 492).

2 - Daftari la wanaostahiki kupewa msada wa pesa na Serikali.

3 - Al Kaamil fit Taareikh (J: 2, Uk: 351).

4 - Siyar A'laami Nnubalaa (J: 3, Uk: 285).

5 - Al Bidaayat Wan Nihaayah (J: 9, Uk: 122), na Tareikhul Islaam (J: 6, Uk: 439).

6 - Al Bidaayat wan Nihaayah: (J: 8, Uk: 146).

7 - Bukhari: (J: 4, Uk: 42), namba (2924).

8 - Al Bidaayat wan Nihaayah (J: 8, Uk: 41).

Ali (Allah maridhie) pembeni mwa Al Ka'ba akasema: **(Huyu ni mtu bora aliye katika ardhi anaependwa na viumbe wa mbinguni)**[1].

(1) NI NANI ALIYEMUUWA HUSEIN (ALLAH AMRIDHIE)?[2]

Katika mwaka wa sitini hijriyyah (60H) Yazid ibn Muawiyah (Allah awaridhie) alipewa Bai'a (kiapo cha utiifu) kuwa Khalifa (wa waislamu), Husein (Allah amridhie) alichukizwa na Bai'a hii; kwa sababu alikuwa anaona yupo anaestahiki zaidi kuwa Khalifa miongoni mwa Maswahaba wa Mtume ﷺ kuliko Yazid, kwa hiyo Husein (Allah amridhie) hakumpa bai'a Yazid (Allah amridhie), aliwaacha watu na jambo lao na yeye akahamia Makkah kwa ajili ya kumwabudu Allah pekee.

Watu wa (Mji wa) Kufa walipata habari kwamba Husein ibn Ali رضي الله عنه hakutoa Bai'a, na kabla ya hapo walikuwa ni watu wenye historia iliyojaa Fitna na (kupenda) Ugomvi, na wakidhihirisha kumili kwa Ali رضي الله عنه na wafuasi wake; kwa hiyo watu wa Kufa walituma barua (nyingi) kwenda kwa Husein رضي الله عنه wakimwita ili wampe Bai'a.

Zilifululiza barua hizo mpaka zikafikia zaidi ya barua (500), wakati huo Husein رضي الله عنه alimtuma Muslim ibn 'Aqil رضي الله عنه mtoto wa 'Ami yake kwenda (Mji wa) Kufa ili kuchunguza habari hii.

Muslim ibn 'Aqil (Allah amridhie) aliingia Mji wa Kufa akawakuta watu wanamtaka Husein (Allah amridhie), ikawa anachukua Bai'a kwa (niaba ya) Husein (Allah amridhie) kwenye nyumba ya Haani' ibn 'Urwa, mpaka ikafika idadi ya waliompa Bai'a miongoni mwa watu wa Kufa ni (18,000), na inasemekana (30,000), baada ya hapo Muslim ibn 'Aqil (Allah amridhie) alimwandikia Husein (Allah amridhie) barua ya kwamba: **[Njoo kwani imekamilika bai'a kwa ajili yako]**.

Habari ilipofika kwa Yazid ibn Muawiya رضي الله عنه (Allah awaridhie) kwamba watu wa Kufa wamempa Bai'a Husein (Allah amridhie) alimpa amri Gavana wake wa (Mji wa) Basra 'Ubaidullahi ibn Ziyad ya kutawala pia Mji wa Kufa, na akamwamrisha awazuie watu wa Kufa pamoja na Husein (Allah amridhie) wasitoke chini ya twaa yake, wala Yazid hakuamrisha kuuawa Husein (Allah amdhie) isipokuwa alitoa amri ya kuzuiliwa asiingie katika (Mji wa) Kufa.

Wakati Muslim ibn 'Aqil رضي الله عنه alipofahamu ya kwamba Ubaydullah ibn Ziyad anataka kutawala Kufa; aliondoka pamoja na watu (4,000) katika waliompa Bai'a miongoni mwa watu wa Kufa kwenda kuizingira Ikulu ya Ubaydullahi ibn Ziyad, na akasisitiza kufanya hivyo.

Ama Ubaydullahi ibn Ziyad kwa hila na ujanja wake alifahamu jinsi gani atalitenganisha jeshi la watu wa Kufa na Muslim ibn 'Aqil; akapeleka ujumbe kwa wakuu wa Makabila ya Kufa na akawapa wao mali itayowafanya washindwe kumpa nusra Husein ibn Ali na Muslim ibn 'Aqil رضي الله عنهما.

Watu wa Kufa (vibaraka wa pesa) wakaanza kuondoka na kutawanyika

---

[1] - Siyar A'laami Nnubalaa: (J: 3, Uk: 275).

[2] - Al Bidaayt wan Nihaaya: (J: 1, Uk: 171), Taarekhur Rusul wal Muluuk (J: 3, Uk: 333) na Man qatalal Husein, cha Abdullahi ibn Abdil Aziz.

huku wakimwacha Muslim ibn A'qilﷺ, mpaka kufikia jioni hakuna mtu hata mmoja aliye pamoja nae.

Muslim ibn 'Aqilﷺ akaangukia kwenye mtego wa ibn Ziyad, na (ibn Ziyad) akatoa amri ya kuuawa, (Muslim) aliandika barua kwenda kwa Huseinﷺ) inayosema: **[Rudi kwa jamaa zako, wasikudanganye watu wa Kufa; hakika wamenidanganya mimi na wewe, na hakuna ahadi kwa mtu mwongo].**

(2) NI NANI ALIYEMFANYIA KHIYANA HUSEIN (ALLAH AMRIDHIE)?

Ama Husein ibn Aliﷺ hakuwa anajua yale yaliyompata mtoto wa Ami yake na khiyana waliyofanya watu wa Kufa dhidi yake, akatoka hali ya kudhani kwamba Bai'a imekamilika kwa ajili yake.

Huseinﷺ alitoka pamoja na watu (70) katika watu wa nyumbani kwake, wakiwemo watoto, ndugu, na watoto wa ndugu zake.

Maswahaba (Allah awaridhie) walijaribu kumrudisha na kumzuia asiende) lakini walishindwa, bali Abdullahi ibn Umar ibnil Khattwaabﷺ alimfuata baada ya kuondoka Huseinﷺ kwa siku tatu, na alipokutana nae alimuuliza: **[Unaelekea wapi?]**, akajibu: **[Naelekea Iraq, na hizi ni barua zao pamoja na Bai'a yao]**, ibn Umar akamwambia: **[Tafadhali usiende]**, lakini Husein alikataa, ibn Umar (Allah amridhie) alipoona ya kwamba Husein amekataa kurudi alimkumbatia na akasema: **[Nakuweka kwenye dhamana ya Allah (wewe) ni miongoni mwa wenye kuuawa]**.

Huseinﷺ aliendelea na safari yake kuelekea nchini Iraq, wakati akiwa njiani alifahamu (habari ya) kuuawa kwa ibn Ami yake Muslim ibn 'Aqilﷺ akatamani kurudi, isipokuwa watoto wa Muslim ibn 'Aqilﷺ waliokuwa pamoja nae walitaka kulipa kisasi kwa baba yao, alikubali rai yao na akandelea na safari.

Ama Ubaydullahi ibn Ziyad alipeleka jeshi lake kwenda kumzuia Huseinﷺ asiingie Mji wa Kufa, makundi hayo mawili yalikutana katika ardhi ya Karbala (10/ Muharram / 61H); Huseinﷺ pamoja na watu (70), na jeshi la ibn Ziyad lenye watu (5,000) likiongozwa na Shamru ibn Dhil-Jaushan na Umar ibn Sa'd.

Husein ﷺ alifahamu ya kwamba hakuna uwiyano baina yake na adui zake; akawataka moja ya mambo matatu:

1- Wamuache arudi alikotoka (Makka).

2- Au aende kwenye mapango ya waislamu kwa ajili ya jihad.

3- Au aende kwa Yazid ibn Muawiya (Allah amridhie) (Sham).

Shamru (aliyekuwa mfuasi wa Aliﷺ lakini leo yuko dhidi yake) alikataa, akataka (Huseinﷺ) akamatwe na afungwe akiwa mateka, na awe chini ya hukmu ya Ubaydullahi ibn Ziyad au (aingie kwenye) mapigano; Huseinﷺ akasema: **[Wallahi sikubali kuwa chini ya Ubaydullahi milele],** kisha jeshi likapanga safu kwa ajili ya vita.

Hapo Huseinﷺ alinyanyua mikono yake mbinguni na kuwaombea dua mbaya watu wa Kufa, akasema: **[Ewe Allah ukiwaacha hai mpaka mwisho wa muda (wao) wagawe makundi makundi, na wawe njia mbali**

mbali, na usimridhie yeyote katika mtawala wao milele; kwa sababu wao wametuita ili watupe nusra kisha wametufanyia uadui na kutuua]. Dua hii imetajwa vilevile kwenye vitabu vya Shia (ithnaasharia)[1]].

Vita ikaanza na yakawa makali mapigano, kwa hakika ilikuwa ni siku ngumu sana kwa Husein؈; kwa sababu ya kuwaona ndugu zake wakianguka mbele yake hali ya kuwa wamekufa, mpaka akabaki peke yake, alitoka Shamru ibn Dhil-Jaushan na kumfuata, akamchoma kwa mkuki shingoni, kisha Husein؈ akaanguka na kufariki.

Hivi ndivyo alivyouliwa bwana wa waislamu zama hizo, ambaye ni mjukuu wa Mtume ﷺ, Mtu wa ibada, Mwenye kupa-nyongo dunia, Aliye bashiriwa pepo, na ni bwana wa waislamu katika wakati wake.

Baada ya kuelezea namna alivyouawa Husein؈ kuna swali muhimu sana linapatikana:

Ni nani aliyemuua Husein؈?, Ni Mashia, Sunni, Bani Umayyah (kama wanavyodai Mashia), au ni watu wengine?.

(3) UKWELI AMBAO MASHIA WANAUFICHA:

Hakika ukweli ambao hakuna budi kila mmoja kujua ni kwamba: waliomuua Husein؈ ni watu wa Mji wa Kufa, ambao walimwita kwa ajili ya kumpa Bai'a kisha wakamfanyia khiyana.

Na ili maneno haya yasibaki kuwa ni tuhuma tu; tutauliza vitabu vya mashia kuhusu tukio hili ili vithibitishe kwamba wale waliomwita Husein؈ ili wampe Bai'a ndio waliomuua, kisha wakatiririsha machozi kwa ajili kifo chake!.

Amesema Sayyid Muhsin Amin: **[Watu (20,000) wa Iraq walimpa Bai'a Husein (Allah amridhie) kisha wakamfanyia khiyana, wakamuua na hali ya kuwa Bai'a yao iko juu ya shingo zao]**[2].

Na amesema Abbas Al Qummiy: **[Zilifululiza barua kwenda kwa Husein (Allah amridhie) mpaka zikakusanyika kwake kwa siku moja zaidi ya barua (600) kutoka kwa (watu) wasiotekeleza ahadi]**[3].

Na mshia Al Ya'qub ametaja ya kwamba wakati Ali ibn Husein؈ alipoingia Mji wa Kufa aliwaona wanawake wanalia na kupiga kelele, akasema: **[Wanatulilia sisi, kwani ni nani aliyetuua?!]**[4].

(4) MSIMMO WA WA AHLUS SUNNAH:

Ama Ahlus Sunnah Wal-jama'ah wanahesabu tukio la kuuawa kwa Husein؈ kuwa ni msiba mkubwa, na ni jeraha baya sana katika Umma, na kwamba wale waliomuua ni viumbe waovu na wenye shari zaidi.

Amesema sheikhul islaam ibn Taymiyyah (Allah amrehemu): **[Ama yule aliyemuua Husein (Allah amridhie), aliyesaidia, na aliyeridhia kuuawa**

---

1 - Al Irshaad: (Uk: 241) cha Al Mufid, na I'ilaamul Waraa: (Uk: 949) cha At Twabrasy, Maa'limul Madrasatayn: (Uk: 128) cha Murtadhwa Al A'skary, na Lawaai'jul Ashjaani (Uk: 188) cha Muhsin Al Amin.

2 - A'ayaanus Shiia: (J: 1, Uk: 34).

3 - Muntahal Aamaal: (J: 1, Uk: 43).

4 - Kitabu: Taareikh: (J: 1, Uk: 235) cha Al Ya'quub.

kwake; ni juu yake laana ya Allah, Malaika na watu wote, hakubali Allah kwake (ibada ya) faradhi wala Sunna][1].

Na Ahlus Sunnah wanajifariji kwa kuwa Husein aliishi kwa wema, na amekufa hali ya kuwa ni shahidi, na hawasemi ila chenye kumridhisha Mola wao, **hawajipigi kwenye mashavu, hawachani nguo, na wala hawafanyi mambo ya Jaahiliyyah**.

Huu ndio msimamo wa Salaf (wema waliotangulia) katika Umma huu kuhusu kuuawa kwa Husein na waliouawa kabla yake; kama Ali ibn Abi Twalib, Uthman ibn Affan na Umar ibnil Khattwab (Allah awaridhie).

(5) BIASHARA YA DAMU YA HUSEIN (ALLAH AMRIDHIE):

Miongoni mwa jambo ambalo hakuna budi waislamu kulijua ni kwamba mashia pamoja na kuendeleza kwao kumbukumbu za kuuawa kwa Husein; ni kuwa wanaiendeleza bidaa hii kwa malengo makuu mawili:

Moja: kuendeleza kukoleza cheche ya ushia kwenye mioyo ya wafuasi wao, na kuyafanya madhehebu yao yaendelee kudumu na kubaki.

Anasema imamu wao wa zama hizi Khomeini: **[Hakika kumlilia shahidi (Husein) huzingatiwa ni kuamsha na kuchochea Mapinduzi]**[2].

Na amesema: **[Kwa kukumbuka misiba yao ndio kumefanya dini ibaki kuwa hai kwa Umma huu]**[3]Na makusudio ya dini hapo ni Ushia Raafidhwah.

Kwa hiyo tumefahamu mafungamano yaliyo baina kumbukumbu (ya kuuawa Husein, na kubaki kwa Mapinduzi ya Iran yaliyofanywa na Khomeini, kisha kuyatangaza katika Ulimwengu wa kiislamu, kwa hiyo mradi wa kisiasa wa Khomeini unatumia fursa ya tukio la kuuawa kwa Husein kujipanua na kujipatia faida nyingine.

Mbili: kuijaza mioyo chuki, na kuzichochea nafsi ili ziendelee kuwachukia maadui wa Ahlul bayt (kama wanavyodai).

(6) NI NANI MAADUI WA AHLUL BAYT?

Kwa mtazamo wa Ki-shia adui wa Ahlul bayt ni yule asiye amini Uimamu.

Shia wanapaza sauti katika siku hiyo kwa kusema: **[kulipa kisasi kwa Husein (Allah amridhie), kulipa kisasi kwa haki ya Ahlul bayt, kwani wako wapi waliomuua Husein (Allah amridhie)?]**, hakika zama zimewamaliza.

Ibnul 'Alqamiy alimhadaa mtawala wa Bani Abbas na kupora (Mji wa) Baghdad kwa kisingizio cha (kulipa) kisasi kwa Husein .

Na pia Ismail As Swafawiy aliwaua watu wa Iraq, (na kumwaga damu nyingi) mpaka akatengeneza kwao Michirizi ya damu kwa kisingiizo cha (kulipa) kisasi kwa Husein.

Na Shia Raafidhwah katika kila zama wanaendelea kumwaga damu ya Ahlus Sunnah kwa kisingizio cha kulipa kisasi kwa damu ya Husein.

Na katika zama hizi nchini Iraq, Sham na Yemen Misikiti inavunjwa, watu wanauawa na kuchomwa moto miili yao, na wanawake wanabakwa kwa kisingizio cha kulipa kisasi kwa ajili ya Husein.

---

1 - Majmuul Fataawa: (J: 4, Uk: 487).

2 - Nahdhwatu 'Aashuraa: (Uk: 8).

3 - Nahdhwatu 'Aashuraa: (Uk: 24).

Na kila (mwaka katika) mwezi wa Muharram Shia Raafidhwah wanazidi ujasiri na ukatili kwa Ahlus Sunnah, na watu wote wanajua kwamba mashairi yanayoimbwa siku ya 'Ashuraa kwa hakika ni sindano ya kujaza chuki kwenye nafsi za wafuasi (wa dini ya Ushia) dhidi ya Ahlus Sunnah Wal-jama'ah.

Amesema Khomein: **(Lazima katika siku ya 'Ashuraa kukumbusha Misiba na dhulma zinazofanywa na madhalimu katika kila zama, hasa katika zama hizi zilizojaa dhulma katika ulimwengu wa kiislamu, kupitia mikono ya wa- Amerika, Urusi na Mawahabi)**[1].

Shia (Rafidhwah) wamelifanya tukio la kumlilia Husein (Allah amridhie) kuwa ni biashara ya (kuuza) damu yake; ili kutimiza malengo ya ki-siasa; kila ikifika siku ya 'Ashuraa viongozi wao huwafuata waislamu na kuwaonesha kuwa wao ndio wakombozi na watetezi wa kadhia za Umma huu, na wakombozi wa maeneo yao matukufu, na ardhi iliyoporwa (hali ya kuwa si kweli).

Watu wote wanajua, na historia ni shahidi ya kwamba (Shia) Raafidhwah hawajawahi kuwa ni sababu ya kupata nguvu waislamu, na wala hawana historia yoyote inayotajwa katika kuiteka Miji (ya Makafiri), wala kukomboa maeneo matakatifu ya waislamu, bali wao ni Upanga unaochoma kwenye miili ya waislamu, na ni Miba yenye kuchochea Mfarakano baina ya waislamu.

Inapasa kwa mwenye akili ajiulize: je kuhuisha (kumbukumbu) za 'Ashuraa na kuchochea nafsi za wafuasi (wa Shia) mbele ya waislamu wengi wa Ahlus Sunnah, (huku) ni kutumikia umoja wanaounadi Mashia usiku na mchana?!

Je huzuni pamoja na kuwalea wafuasi juu ya kuwatusi na kuwalani wabora wa umma huu (Maswahaba), yanaleta mafungano mazuri baina ya Shia na Sunni au ni kuwasha moto, na kuamsha fitina iliyolala?! **Fitna imelala amelaaniwa mwenye kuiamsha**[2].

Je kupaza kwao sauti kwa vilio, kujipiga kwa minyororo na mapanga vichwani na migongoni ni ujumbe wa amani kwetu? Au wanatumia taqiyyah[3] lakini wana njama za uhalifu dhidi yetu?. Uhalisia unaashiria kwenye jambo la pili.

Wabillahi Ttaufiq

Ewe Allah ilinde miji yetu na miji ya waislamu na kila shari na ubaya, na tuepushe na fitna zenye kudhihiri na kujificha.

Abu Halima Arafat

13 rajab 1438H - 10/4/2017M

Tanzania.

---

1 - Nahdhwatu Aa'shuraa: (uk: 109).

2 - (Fittna imelala na Allah amlani Yule mwenye kuiamsha). si hadithisahihi.

3 - Mashia wana itikadi ya Taqiyyah nayo ni: (kudhihirisha kinyume na unavyoitakidi).